

**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO**  
**SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS (S. 3874)**

S.L.P. 6083 – Morogoro  
Simu 0689-783630 (Ofisi Taaluma) / 0789-978886 (Airtel Money)  
0689-783672 (Bweni la kike) / 0689-782670 (Bweni la kiume)  
www.alfashule.ac.tz

**TARATIBU ZA KUJIUNGA NA MASOMO YA JIONI**

Ndugu, umeomba nafasi ya kujiunga na masomo ya jioni kwenye shule yetu iliyoko katika manispaa ya Morogoro, kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

**Ada ni:**

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 400,000 kwa mwaka. Ilipwe kwa mkupuo mmoja.
- (b) Kwa msichana wa bweni Tsh. 1,000,000 kwa mwaka. Ilipwe awamu ya kwanza Tsh. 600,000, halafu Tsh. 150,000 mara tatu (Machi, Juni na Agosti). Bweni halina nafasi kwa wavulana; watakaolihitaji wanashauriwa kusoma katika kituo chetu Tumaini Letu kilichopo Kihonda Azimio.

Ukitarajia kufanya mtihani wa taifa mnamo Novemba, uandae mapema ada yake pia iweze kutumwa kwa Baraza la Taifa kwa wakati uliopangwa, usije ukadaiwa faini, lakini usiichanganye na ada ya shule.

Kwa usalama wa wote unaombwa **ulipie benki** (akaunti yenye jina la shule iko MKOMBOZI C.B. ikiwa na namba 00120603517801; iko pia CRDB, namba 01J2077746000) **halafu vocha uilete shuleni** katika ofisi ya mhasibu upate risiti. Nje ya hapo usitoe pesa kwa yeyote, hata kama ni mwalimu wetu: malipo ya namna hiyo si halali, hivyo shule haihusiki nayo. Jihadhari sana!

Shule imekubaliwa pia kuwa wakala wa Airtel Money kwa ajili ya kutuma pesa kwa urahisi zaidi. Namba ni 0789-978886 na inatumika kwa mawasiliano na kwa kutuma pesa. Vilevile shule imekubaliwa kuwa wakala wa benki ya Mkombozi, tena utaratibu wa kuwa wakala wa CRDB unakaribia kukamilika.

Bila kutimiza malipo yote yanayotakiwa hutapokewa. Tena ukichelewa kujisajili kwa malipo utakosa nafasi yako.

**Masomo yataanza tarehe 2-1-2024.**

- (a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufike shuleni tarehe hiyo saa 8:00 mchana.
- (b) Ukitaka kukaa bweni ufike kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa wasichana waliowahi kuleta vocha ya benki hata kabla ya tarehe hiyo; tunasisitiza kwamba kwa wavulana hakuna).

Ulete Biblia (isipokuwa kama si Mkristo au utasoma kwetu mwaka mmoja tu), kamusi ya Kiingereza, kivuli cha cheti cha kumaliza masomo na vitu vilivyoorodheshwa hapa chini:

- (a) Kwa wasichana:
  - (i) Fulana yenye maandishi ya shule
  - (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie sentimeta 25 kutoka ardhini)
  - (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
  - (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
  - (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
  - (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
  - (vii) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika
- (i) Fulana yenye maandishi ya shule
- (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
- (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
- (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
- (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
- (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya shule, bukta ya buluu na raba
- (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya shirika.

b) Kwa wavulana:

- 2. Kwa kukaa bweni (wasichana tu):
  - (a) Fulana ya kijani yenye maandishi ya shule
  - (b) Sketi nyeusi (ifikie sentimeta 25 kutoka ardhini)
  - (c) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
  - (d) Mashuka na blanketi
  - (e) Chandarua kilichotiwa dawa
  - (f) Godoro la futi mbili unusu
  - (g) Ndoo
  - (h) Sanduku imara na salama
  - (i) Taulo na vifaa vingine vya usafi
  - (j) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
  - (K) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote.

**N.B. Ni lazima** mashati, fulana za shule, sketi, suruali na sweta vinunuliwe shuleni.

Biblia (Tsh. 25,000), kamusi (Tsh. 25,000), magodoro (Tsh. 42,000), mablanketi (Tsh. 15,000), mashuka (Tsh. 7,000), vyandarua (Tsh. 6,000), trakisuti (Tsh. 18,000), taulo (Tsh. 6,000), ndoo (Tsh. 3,500), madaftari na kalamu vinapatikana shuleni kwa bei nafuu kama ilivyoonyeshwa katika mabano.

